**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# OFISI YA RAIS

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MPANGO WA UFUNDISHAJI WANAFUNZI WA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI KWA NJIA YA VIPINDI VYA TELEVISION, RADIO NA MITANDAO ILIYOTOLEWA NA MHESHIMIWA SELEMANI S. JAFO (MB.), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS - TAMISEMI - TAREHE 29 APRILI, 2020**

**29 APRILI, 2020**

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MPANGO WA UFUNDISHAJI WANAFUNZI WA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI KWA NJIA YA VIPINDI VYA TELEVISION, RADIO NA MITANDAO

## 1.0 UTANGULIZI

**Ngudu Waandishi wa Habari,**

Nachukua fursa hii kuwakaribisha katika Wizara yetu siku hii ya leo. Nimewaita ili tuweze kupeana taarifa kuhusu mpango unaoendelea wa ufundishaji wa wanafunzi wetu wa Shule za Msingi na Sekondari kwa njia ya vipindi vya Televisheni, Radio na Mitandao ya kijamii.

Sote tunafahamu kuwa nchi yetu inapambana na changamoto ya kuzuia kusambaa kwa maambukizi ya Homa ya Mapafu inayosababishwa na Virusi vya Corona (COVID-2019). Kufuatia hilo, hatua mbalimbali zilichukuliwa na Serikali ikiwa ni pamoja na kuzifunga shule zote kuanzia shule za awali hadi vyuo vikuu nchini. Kufungwa kwa shule licha ya kwamba umelenga kuwalinda watoto wetu na maambuzi ya Virusi vya Corona, kumeleta changamoto ya watoto wetu kukosa fursa ya kufundishwa masomo na walimu wao kwa mujibu wa mihula ya shule/vyuo ilivyokuwa inatekelezwa.

Aidha, baadhi ya wanafunzi walikuwa katika maandalizi ya Mitihani ya Taifa ambapo fursa ya kujiandaa kwenye mitihani ilikumbana na changamoto hiyo ikiwa ni pamoja na kuahirishwa kwa Mitihani ya Kidato cha Sita na Ualimu iliyokuwa ifanyike kuanzia tarehe 4 Mei, 2020; hadi hapo itakapotangazwa baadae, baada ya changamoto tuliyonayo itakapopungua au kuondoshwa kabisa.

**Ndugu Waandishi wa Habari**

Serikali inatambua kuwa kufungwa kwa Shule za Msingi na Sekondari katika Serikali za Mitaa kulileta taharuki kwa wanafunzi wetu, wazazi na walezi, walimu na wadau kwa ujumla kuhusu mustakabali wa usomaji wa wanafunzi na elimu katika Taifa letu. Aidha, Wazazi wengi walikuwa wakilalamika kuhusu ugumu wa kuwadhibiti watoto wao nyumbani kwa

kutokana na wanafunzi hao kukosa kazi za kufanya na hivyo baadhi yao kuendelea kukutana na wenzao mitaani; jambo ambalo lilizidi kuongeza uwezekano wa watoto wetu kuambukizwa na Virusi vya Corona.

## 2.0 UFUNDISHAJI WANAFUNZI WA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI WAKIWA NYUMBANI

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Mtakumbuka hivi karibuni Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia kwa Katibu Mkuu wake ilizindua mpango wa Serikali ulioratibiwa na **Taasisi ya Elimu Tanzania** na **Baraza la Mitihani la Tanzania** wa kuwafundisha wanafunzi wa Darasa la Kwanza hadi Kidato cha Sita kupitia Televisheni, Radio na Mitandao ya Kijamii.

Tangu wiki iliyopita tumeshuhudia vipindi vya masomo mablimbali na kwa ngazi mbalimbali za Elimu Msingi na Sekondari vikirushwa kwenye Televisheni za Azam, ZBC na Chanel Ten. Aidha, Jumatatu **27 Aprili, 2020**, tumeshuhudia pia Televisheni yetu ya Taifa (TBC) ikianza rasmi kurusha vipindi vya marudio na maandalizi ya Mitihani ya Taifa kwa wanafunzi wetu wa Kidato cha Sita.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Nimefurahishwa sana na jinsi ambavyo utatuzi wa changamoto ya kuwawezesha wanafunzi wetu wa Shule za Msingi na Sekondari katika Serikali za Mitaa kupata masomo kupitia Televisheni, Radio na Mitandao. Kilichonifurahisha zaidi ni namna ambavyo **suluhisho la changamoto** hii kubwa na iliyotupata ghafla bila kutegemea na wala kujiandaa imepatiwa ufumbuzi wa haraka kwa kuratibiwa na Watanzania wenyewe ***(Local Initiatives).***

Taasisi zetu za Serikali za **Baraza la Mitihani** na **Taasisi ya Elimu Tanzania** zilibuni mipango kabambe ambayo Wizara zetu za sekta ya Elimu tuliona ni mipango mizuri na ya kimapinduzi kutekelezwa katika taifa letu. Ubunifu huu wa Taasisi zetu kuweza kushirikisha wadau mbalimbali wa Sekta Binafsi umewezesha kufanikisha kuanza kutekelezwa kwa mpango wa ufundishaji wa wanafunzi wetu wa Shule za Msingi na

Sekondari wakiwa nyumbani. Aidha, ushiriki wa Sekta binafsi kwa namna moja au nyingine kufanikisha hili, umeonesha jinsi ambavyo ushirikiano wa Serikali yetu na Sekta Binafsi (PPP) ulivyoimara na unavyoweza kuleta ufanisi mkubwa wa utatuzi wa changamoto zinazoweza kutukabili wakati wowote.

## 3.0 PONGEZI KWA WARATIBU WA MPANGO NA WASHIRIKI WAKE

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Nitumie fursa hii kupongeza kwa dhati ya moyo wangu watendaji wote wa Baraza la Mitihani la Tanzania na Taasisi ya Elimu Tanzania kwa kubuni, kuanzisha na kuratibu mipango ya Taasisi hizo ya kuwafundisha wanafunzi wa Elimu ya Msingi na Sekondari kwa njia ya Televisheni, Radio na Mitandao. Aidha, napongeza sana utaratibu wa kuwawezesha wanafunzi wanaokabiliwa na Mitihani ya Taifa wa Kidato cha Sita kufanya marudio na maandalizi thabiti ya Mitihani yao kupitia televisheni ya taifa.

Niwapongeze sana walimu wetu wa Shule za Msingi na Sekondari walioshirikishwa na Baraza la Mitihani na Taasisi ya Elimu Tanzania kushiriki kwa niaba ya wenzao kuwasilisha mada za masomo mbalimbali kwa ngazi tofauti kwa wanafunzi wetu. Mchango wenu kwa Taifa tunauheshimu sana na ninawashukuru na kuwapongeza sana kwa kazi mnayoendelea kuifanya. Najua bado mnaendelea na maandalizi ya vipindi vinavyoendelea na hivyo nawatia moyo muendelee kwa jitihada zote kuelimisha wanafunzi wa Taifa letu kupitia mpango huu.

Nimefarijika pia kupata taarifa kuwa **Chama cha Walimu Tanzania (CWT)** kiliunga mkono na kusaidia mpango wa Baraza la Mitihani kuwawezesha walimu kupewa mafunzo maalumu na Baraza la Mitihani yaliyowawezesha kuandaa vipindi vya marudio na Maandalizi ya mitihani kwa wanafunzi wa Kidato cha Sita. Nawashukuru sana na kuwapongeza sana Viongozi wa CWT, walimu wote nchini kwa msaada huu mlioutoa wenye tija kubwa kwa mustakabali wa elimu ya wanafunzi wa Taifa letu.

Nimefahamishwa pia **Global Education Link** imeweza kusaidia kusimamia uandaaji wa vipindi vilivyoandaliwa na Baraza la Mitihani kwa kutumia rasilimaliwatu na fedha kuhakikisha wanafanikisha mpango wa Baraza la

mitihani wa kuwaandaa wanafunzi kwa madarasa yanayokabiliwa na mitihani ya taifa kwa mwaka 2020. Ninawashukuru sana na kuwapongeza Global Education Link na kuwaomba muendelee kusaidia siku zote na msirudi nyuma kamwe.

Ninaishukuru **Taasisi ya Elimu Solution** kwa ushiriki wao mzuri katika masuala ya kuwasaidia vijana wetu kielimu.

Ninatambua katika kufanikisha kazi kubwa inayofanywa na Taasisi ya Elimu Tanzania kuandaa masomo ya madarasa mbalimbali ya Msingi na Sekondari imeungwa mkono na wafadhili mbalimbali. Ninawashukuru sana na kuwapongeza katika kufanikisha mpango kabambe wa kuwafundisha wanafunzi kwa ngazi za elimu ya Msingi na Sekondari. Nawashukuru na kuwapongezi sana Wafadhili wote waliotusaidia.

Ninatambua kuwa pamoja na maandalizi ya vipindi hivi yaliyofanywa na yanayoendelea kufanywa na Baraza la Mitihani na Taasisi ya Elimu Tanzania, yamefanikishwa na uzalendo mkubwa na uungwaji mkono wa vyombo vyetu vya habari nchini. Nawashukuru sana na kuwapongeza kwa dhati Televisheni zetu, TBC, Azam, ZBC, Chanel Ten na Radio zetu za Taifa, Kanda na Mikoa. Kazi mlizofanya ni nzuri sana katika kuunga mkono jitihada za Serikali yetu kuwezesha wanafunzi wetu kuendelea na masomo yao katika kipindi hiki ambacho Serikali inapambana na kudhibiti maambukizi ya Virusi vya Korona.

## 4.0 WITO KWA WANAFUNZI, WAZAZI NA WADAU

**Ndugu Waandishi wa habari,**

Niimefuatilia kwa umakini juu ya kazi kubwa ambazo zimefanywa na walimu wetu katika ufundishaji kwa ujumla kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania na Baraza la Mitihani la Tanzania. Nimejionea jinsi walimu wetu wanavyoeleweka vizuri, wanafundisha kwa umahiri mkubwa na wanazingatia nidhamu za ufundishaji. Aidha, nimeshuhudia walimu wakiwashirikisha wanafunzi namna ya kujibu maswali mbalimbali yenye kupima umahiri kwa wanafunzi wa Kidato cha sita. Kwa msingi huo, natoa wito kwamba;

## 4.1 Wito Kwa Wanafunzi

- Wote wazingatie kutulia Nyumbani na kusoma kwa bidii.
- Wanafunzi wote wazingatie ufuatiliaji wa ratiba za masomo yao kama zilivyopangwa.
- Wanafunzi wafanye maswali ambayo walimu wamewapatia kama mazoezi.
- Wanafunzi waulize maswali kwa kutumia *Email* elekezi katika kipindi husika; Ama watume maswali kwa kupitia namba za simu ambazo zinaonekana katika Luninga wakati kipindi kinaendelea.
- Ikiwa kipindi hukukielewa vizuri wakati wa kukiangalia kwenye Luninga, ama kimekupita kwa bahati mbaya ama ulichelewa ukakuta kimekwisha anza na hivyo ukawa unataka kukirudia tena, jua vipindi vyote vinapatikana katika YOUTUBE elekezi ambazo zitakuwa zikitolewa wakati kipindi kinaendelea ama katika miongoni mwa linki zilizoorodheshwa hapo chini.

## 4.2 Wito Kwa Wazazi

- Mzazi hakikisha Mwanao anapata muda wakutosha na kufuatilia masomo haya.
- Familia zijiepushe kumwingiza mwanafunzi katika kufanya biashara/kazi nyingi za Familia ambazo zinaweza kumfanya akashindwa kufuatilia vipindi hivi.
- Hakikisha Mzazi anatoa msaada wezeshi wa usomaji katika mazingira rafiki nyumbani ili mwanafunzi aweze kufikia malengo.
- Mzazi hakikisha mwanafunzi anafanya mazoezi ya darasani anayokuwa amepewa na walimu wakati kipindi kinaendelea
- Mzazi hakikisha mwanafunzi anafuatilia vipindi hivi kwa njia ya Television ama Simu ya mkononi kwa kupitia mtandao wa (Youtube).

### 4.3 Wito Kwa Baraza La Mitihani

Muendelee na jitihada zenu za kuhakikisha vipindi vya marudio na maandalizi kwa wanafunzi wanaokabiliwa na Mitihani ya Taifa vinakamilishwa na kufundishwa kwa wanafunzi. Jitihada za Baraza la Mitihani zifanikishe pia maandalizi ya madarasa ya mitihani ya Darasa la Nne, la Saba, Kidato cha Pili na Kidato cha Nne.

### 4.4 Wito Kwa Taasisi Ya Elimu Tanzania

Natambua kazi kubwa mnayoendelea nayo kufanikisha upatikanaji wa vipindi kwa madarasa mbalimbali ya Shule za Msingi na Sekondari, muendelee na juhudi hiyo ili kuendeleza mafanikio haya yanayoendelea kupatikana kwa wanafunzi wetu nchini.

### 4.5 Wito Kwa Wadu Mbalimbali Wa Elimu

Nichukue nafasi hii kuwashukuru kwa dhati Wadau mbalimbali ambao wamejitokeza tangu mwanzo na kushirikiana na Serikali katika kuhakikisha jambo hili limefanikiwa kwa hatua za kuanzia.

Vyombo mbalimbali vya habari ikiwepo Shirika la Habari la Taifa TBC, ZBC, AZAM-TV, CHANNEL 10, CLOUDS FM, GLOBAL TV, GEL TV na Radio mbalimbali na wengine ikiwa nimewasahau, niwaombe tuendelee kushirikiana katika kipindi hiki kigumu cha COVID-19 kwa kuwasaidia wanafunzi wetu waliopo nyumbani.

Nitoe shukrani zangu za pekee kwa **Chama cha Walimu Tanzania (CWT),** Mawakala wa Vyuo Vikuu Nje ya Nchi **Global Education Link (GEL), UNESCO na Taasisi ya Elimu Solution** kwa kazi kubwa ambayo kila mmoja kwa nafasi yake ameweza kusaidia kazi hii, tufahamu ya kuwa bado tunawahitaji sana, kwani kazi iliyopo mbele yetu ni kubwa sana.

Ninaomba Wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi, wajitokeze kuweza kuungana na Serikali katika kipindi hiki kigumu tunachopitia. Nitoe wito kwa Mashirika ya Umma na binafsi wote tuungane kwa pamoja na kusaidia suala hili la upatikanaji wa elimu kwa njia ya Mtandao.

## 5.0 UPATIKANAJI WA VIPINDI

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Wajulisheni wanafunzi pia kuwa vipindi vinavyofundishwa njia ya Televisheni unaweza kuvirejea kupitia mitandao ya ***YOUTUBE*** kwa ajili ya marudio ili kujenga uelewa zaidi. Mitandao hiyo ni pamoja na:

- ✓ Baraza la Mitihani-NECTA
- ✓ Taasisi ya Elimu Tanzania-TAE
- ✓ Global Education Link TV.(GEL TV)
- ✓ GLOBAL TV
- ✓ AZAM -TV
- ✓ ZBC-TV
- ✓ E.A -TV

## 6.0 MWISHO

Ofisi ya Rais - TAMISEMI, inawaasa wanafunzi wote, wazazi, walimu, wadau wa maendeleo wote na jamii kwa ujumla, tuendelee kuchukua tahadhari katika kujikinga na maambukizi ya virusi vya COVID-19, kwa kila mmoja wetu kuzingatia taratibu na maelekezo yanayotoka katika Mamlaka husika.

Uongozi wa OR-TAMISEMI; unawashukuru Wadau wote waliofanikisha kuanza rasmi kwa mpango huu wa mafunzo kwa Wanafunzi wa shule za Sekondari za Tanzania.

**Imetolewa na;**

**Selemani S. Jafo (Mb.)**
**WAZIRI WA NCHI**
**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**